**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 08 Juni, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

122. MHESHIMIWA HABIB ALI MOHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa mujibu wa Sheria za nchi yetu, binaadamu wote ni sawa na wanastahiki kupewa huduma ya matibabu bila ubaguzi wowote. Katika kufanikisha hili, Serikali inawajibu wa kuhakikisha vituo vyote vya afya vina madaktari na wauguzi wa kutosha.

(a) Inawezekana tatizo hili limeenea katika sehemu nyingi. Je, Wizara yako imefanya tathmini maalum kulibaini uhalisia wake.

(b) Je, utakubaliana na mimi kuwa kuna uhaba wa madaktari na wauguzi katika Kituo cha Afya cha Makuungeni Mtambwe Kusini.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

23. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Wananchi wengi wa vijiji vya Pemba bado wanatumia miti katika ujenzi wa nyumba zao za kuishi huku ikifahamika kuwa, ukataji wa misitu husababisha uharibifu mkubwa wa mazingira na mabadiliko ya tabia ya nchi (climatic changes). Hata hivyo, katika kupambana na uharibifu huo mnamo miaka ya 70, Serikali ilianzisha vituo vya kutengeneza matofali ya udongo yaliyojengewa nyumba za Serikali zilizoitwa nyumba za vijiji na hatimae walipewa wananchi kuishi.

Je, ni lini Serikali itarejesha vituo vya kutengeneza matofali ya kuchoma ya udongo ili kuwakomboa wananchi.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

168. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Katika kipindi cha tarehe 07/04/2021, Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini alifanya ziara ya kikazi ya kutembelea baadhi ya maeneo katika jimbo la Wawi kwa lengo la kuangalia changamoto zinazowakabili wananchi juu ya upatikanaji wa maji safi na salama. Miongoni mwa maeneo hayo ni pamoja na Mgogoni, Ditia, Gombani na Kichangani.

(a) Je, Mhe. Waziri katika ziara yako hiyo ni mambo gani umeweza kuyabaini kuhusiana na upatikanaji wa maji safi na salama

(b) Je, ni lini changamoto ya upatikanaji wa maji safi na salama katika jimbo la Wawi itaondoka.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

70. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mradi wa ujenzi wa viwanja vya michezo kwa kila Wilaya. Hata hivyo, kwa Wilaya ya Magharib "A" kiwanja kilichopangwa kujengwa katika Shehia ya Kama, bado ujenzi wake haujaanza.

(a) Je, ni sababu gani za msingi zinazosababisha ujenzi wa kiwanja hicho kuchelewa kuanza.

(b) Ni kiasi gani cha fedha kinachotarajiwa kutumika katika ujenzi wa kiwanja hicho.

(c) Yapo malalamiko kwamba baadhi ya viwanja vilivyojengwa havikufikia ubora uliokusudiwa. Je, Serikali imejiandaa vipi ili kiwanja cha Kama kifikie kiwango.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

205. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Suala la matengenezo ya meli ya MV. Mapinduzi na matumaini ya kurudi na kuendelea kufanya safari zake kama ilivyokuwa awali limekuwa na mkwamo wa muda mrefu ikizingatiwa pia bado Serikali inaendelea kupata hasara.

(a) Je, ni ipi ahadi ya Serikali kuhusiana na hatima ya meli hiyo.

(b) Je, Serikali ina njia gani mbadala ya kuweza kunusuru hasara inayoingia katika kuihudumia meli hiyo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

138. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Watoto waliofeli darasa la sita (6) na la kumi (10) hulazimika kurudia tena masomo yao na wengine hukaa zaidi ya mwaka mmoja huku umri wao ukizidi kuwa mkubwa zaidi kuliko wanafunzi wengine wa elimu ya Sekondari.

(a) Je, kwa nini watoto wanapofeli kwa mara ya pili wasipelekwe kwenye Mafunzo ya Amali.

(b) Je, kurudia darasa kwa zaidi ya miaka miwili hakuwapelekei wanafunzi hao kukosa fursa ya kumaliza elimu rasmi.

202. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Umuhimu wa lugha ya Kiengereza katika mawasiliano ya mwanadamu ni sawa na lugha ya Kiswahili, Kiarabu, Kitaliana na Kifaransa. Hata hivyo, lugha ya Kiengereza ina umuhimu wa pekee hasa katika mawasiliano ya Kimataifa.

Je, Wizara yako haioni umuhimu wa kupunguza masomo katika skuli za msingi ili kulijengea umuhimu somo hili.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

177. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Katika shehia ya Shamiani – Mwambe kuna Kituo cha Afya ambacho kwanza ni kibovu na kinavuja wakati wa mvua kutokana na ubovu wake na hakina daktari.

(a) Je, Wizara inalijua hili.

(b) Je, Wizara itachukua hatua gani ili kutatua changamoto hizo.

**Zanzibar,**
**08 Juni, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**